

Rahabu Afuata Maagizo

YOSHUA SURA YA 2 NA YA 6

Chagua mazoezi yanayofaa mahitaji na mapendezi ya mtoto wako. Fanyeni mazoezi hayo mkiwa familia.



SOMA YOSHUA SURA YA 2 NA YA 6

Kisha, soma Hadithi ya Biblia Iliyochorwa (kwenye Intaneti au kwenye karatasi iliyochapishwa), na mzungumzie maswali yaliyo mwishoni mwa hadithi hiyo.


JARIBU KUFANYA HIVI: Sikiliza drama ya sauti inayoitwa *Yehova Hukomboa Wale Wanaoita Juu ya Jina Lake*. Halafu, zungumzieni maswali haya mkiwa familia: (1) Kwa nini Yehova aliokoa Rahabu na Wagibeoni ingawa hawakuwa Waisraeli? (2) Hilo linakufundisha nini kumhusu Yehova? (Soma Zaburi 34:15; Matendo 10:34, 35.) Pakua drama hii katika Tovuti ya www.jw.org/sw. Tafuta kwenye **MACHAPISHO > DRAMA**.

MAZOEZI ZAIDI UNAYOWEZA KUCHAPA



MAZOEZI YA PICHA

JIFUNZE KUCHORA Msaidie mtoto wako amchore Rahabu, kwa kutumia mfano wa mchoro uliopo. Halafu, msaidia apake rangi mchoro huo.



MAZOEZI YA KUJIFUNZA

PATANISHA KADI Baada ya mtoto wako kukata kadi, msaidie atumie madokezo na maandiko kupatanisha kila mhusika katika Biblia kwenye kadi moja kubwa.



KUSANYA NA UJIFUNZE

KADI YA MHUSIKA KATIKA BIBLIA Soma mambo machache kumhusu pamoja na mtoto wako. Uliza maswali yaliyo kwenye kadi. Mkiwa familia, tumia kadi hii na kadi nyingine za wahusika katika Biblia zinazopatikana kwenye Tovuti ya jw.org/sw kutafuta wahusika wawili katika Biblia, mbali na Rahabu, ambao mwanzoni hawakumtumikia Yehova lakini baadaye wakawa waabudu wake: (1) mmishonari aliyewatesa Wakristo awali na (2) mwanamke Mmoabu aliyekuja kuwa nyanya ya Yesu Kristo. —Ruthu 1:22; Mathayo 1:5, 16; Matendo 21:40–22:16.